# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KARATASI YA TATU-102/3 MTIHANI WA MWIGO 2022

## SEHEMU YA A

a. Aina-Mbolezi

-unahusu **kifo**; umeanguka mwamba

-marehemu **amesifiwa**-jabali tuloegemea

-**toni** ni ya huzuni-hangaiko metukumba

-mbona kaacha **mauko** ngoma yetu kuvamia

**-imani** ya jamii kuhusu kifo-Maulana ameacha kifo kuvamia jamii

Kutaja aina=1

Athibitishe kwa hoja tatu 3x1=3

Jumla=4

b. i) jazanda/istiara-umeanguka mwamba; mtu muhimu amefariki, makinda
ii) inkisari-lilotupa, ajua
iii) kuboronga sarufi-mahasidi kutishia, riziki kutuangushia
iv)methali-mti mkuu umegwa
v) swali balagha-wana wa ndege wa wapi?
vi)lahaja-ela
vii) mbinu rejeshi-jabali tuloegemea
za kwanza 5x1=5; atoe mifano.

c.

i. **Kurithisha** kipera hiki kwa vizazi vya sasa na vijavyo.
ii. Kukifanyia kipera hiki **utafiti** ili kubainisha sifa za uwasilishaji wazo na kuzihifadhi
iii. Kukihifadhi kwenye **maandishi.**
iv. **Kukifunza** shuleni
v. **Kuziimba** mara kwa mara/kujifunza uimbaji wake.

vi. Kuhifadhi kwenye **video** ili kuhifadhi sifa za uwasilishaji kama vile suti/kidatu na miondoko.
vii. Kutafitia **vyanzo** vya kudidimia kwazo na kuzidhibiti.
viii. Kuandaa **mashindano** ya uimbaji ili kurithisha utambaji wazo kwa kizazi kingine.
ix. Kushirikisha **wageni** waalikwa katika ujifunzaji wa mbolezi/kujifunza kwa mitindo anuwai ili kuwafanya wanafunzi wavutiwe nazo, na kuziendeleza.
x. Kutumia **kufunzia** masomo mengine na stadi nyingine kama vile kusikiliza na kuzungumza.
xi. Kuandaa **vipindi** vya redio au runinga na kuwaalika mafanani stadi kuimba ili kuwa vielelezo.
xii. Kuelimisha jamii kuhusu **umuhimu** wake.

Za kwanza 4x1

d.

i. Kwa kushiriki, mtafiti huja karibu zaidi na jamii na hupata habari za **kuaminika** moja kwa moja.
ii. Ni njia bora ya kupata habari kutoka kwa watu ambao **hawaju**i kusoma na kuandika ama wale ambao huona vigumu kujieleza moja kwa moja.
iii. Ni rahisi kwa mtafiti **kuuliza** maswali muhimu kuhusu kipera hiki.
iv. Mtafiti anaweza **kunakili**/kunasa anayosikiliza au anayotazama, hivyo kuhifadhi sifa za kiimbo, toni na ishara.
v. Mtafiti hupata taathira na **hisia** halisi ya yanayowasilishwa kwa vile anakabiliana ana kwa ana na watendaji na hivyo kuelewa zaidi.
vi. Mtafiti anaweza **kuthibitisha** yale aliyokusanya kupitia kwa hojaji na mahojiano kwa kuyahakiki.
vii. Kushiriki hukuza **utangamano** kati ya mtafiti na wanajamii.

3x1=3; sahihisha za kwanza tatu.

e.

Aina- Majigambo/kivugo

-anajiita **jogoo** la kijijini
-**linawikia** jijini
-**liloyavunja** makoo ya jijini
-**linasifiwa** na makoo yote
-koo wake ni wa **wafalme**
-wao ni **wakulima**

-yeye **hulima** maekari kwa maekari
-hutumia siku **chache** kulima
-anasakata **kandanda**
-kila mtu **anamfahamu**

Kutaja aina=1
Kuthibitisha=3

## SEHEMU B: RIWAYA

2a) i) Wasemaji ni **viongozi** wa Shirika la Maghala ya Nafaka.

ii) Aliyeambiwa ni **Lunga**.

iii) Alikuwa **amepinga** uuzaji wa mahindi yaliyoharibika.

iv) Mahindi yalitolewa **ng'ambo**

v) Msimamo wa Lunga ulimfanya **kuachishwa** kazi.

vi) **Walisisitiza** kuwa ni lazima watu wapewe mahindi hayo licha ya kuwa yalikuwa mabovu/watu walikuwa **maskini**/wangekufa njaa.

Dondoo limetolewa uk. 71

Zozote 4x1

b) Anayeambiwa maneno haya ni Lunga:

i. Anaendeleza kipengele cha **mgogoro** ambacho ni muhimu katika kujenga ploti. Ana mgogoro na waajiri wake kuhusu mahindi/ na mkewe kuhusu umaskini wake.
ii. **Barua** anayoandikiwa ya kustaafishwa ni kipengele cha ploti. Anaachishwa kazi.
iii. **Hotuba** ya Lunga ni kipengele cha ploti. Anazungumzia suala la mazingira.
iv. **Kumaskinika** kwake kunabadilisha msuko wa riwaya. Mkewe anamtoroka.
v. **Kifo** cha Lunga kinabadilisha msuko wa riwaya. Sauna anawaiba wanawe; Umu anaondoka nyumbani kwenda kupambana na wanawe.
vi. Ametumiwa kusawiri **mabadiliko** katika maisha ya binadamu.Alianza kukata miti. Wahusika wengi pia walibadilika kwa mfano Sauna.

vii. Amesababisha kuibuka kwa **wahusika** wengine kv Kimondo. Walisoma katika darasa moja.
viii. Amechangia katika kuendeleza **ufaafu** wa anwani. Mara nyingi alipata dhiki na faraja. Mkewe alipoondoka alisaidiwa na majirani kutunza wanawe.
ix. Tunafahamu **usuli** wa familia yake kupitia kwake-Mababu zake walihamia katika Mlima wa Simba kutoka Kaoleni.

Zozote 3x2=6

c) Athibitishe kuwa maskini ni mtumwa/hawezi kuchagua:

i. Wahafidhina wanauziwa **mahindi** yaliyoharibika kwa kuwa walikuwa maskini/wangekufa njaa.
ii. Kuna watoto wengi **ombaomba** katika jamii km Hazina.
iii. Watu wanaopora **mafuta** na kujaribu kuokolewa na Makaa wanafia hapo lori linapolipuka.
iv. Maskini wanachukuwa mali zisizo zao. **Wanapora** maduka ya wenzao. Walipora maduka wa Wahindi na hata waafrika wenzao. Watu hawa wanafia katika jumba la Ridhaa.
v. Chandachema anaishi maisha ya taabu baada ya kutoka kwa Bw. Tenge na Bi. Kimai. **Analala** kwenye michai.
vi. Wakimbizi katika mlima wa Mamba wanakula **mizizi** ya mwitu na matunda mwitu kwa mfano Ridhaa.
vii. Wakimbizi hawa **wanang'ang'ania** chakula cha msaada kinapotolewa.
viii. Wakimbizi wanakunywa **maji** machafu kutoka katika Mto wa Mamba.
ix. Dick, kando na kujiingiza katika matumizi na ulanguzi wa dawa za kulevya kutokana na kutishwa na Buda, anataka kukidhi **mahitaji** yake ya kimsingi.
x. Sauna anaingilia biashara mbalimbali **haramu** km ulanguzi wa watoto kutoka na kutomudu maisha yake.
xi. Lunga **anaachishwa** kazi kwa kuwa hana uwezo. Yeye ni mtegemezi asiye na haki.
xii. Pete anaishi maisha ya **taabu** baada ya kifo cha nyanya yake. Anatumiwa na wanaume; wanamzalisha watoto watatu.
xiii. Vijana wa **vyuo** vikuu ni maskini; hela za ufadhili hazitoshi. Wanaingilia matumizi ya pombe haramu.
xiv. Shamsi **anamtegemea** pakubwa mkewe Halua. Anamtegemea kwa chakula.
xv. Babake Shamsi **ananyang'anywa** shamba lake. Anatumikishwa katika shamba lilo hilo.
xvi. Babake Shamsi pia ana anakula **vijasumu** vya mizizi mwitu kutokana na njaa.

Zozote 10x1=10; Kadiria hoja nyingine.

3a

i) Tanakuzi-mwanamke/mwanamme
ii) Jazanda-kulielekeza jahazi hili letu kwenye visiwa vya hazina
iii) Uhuishaji-wale maadui
iv) Swali balagha-je, huu sio uliokuwa muono wa waliopigania uhuru?
v) Mbinu rejeshi-waliochukua hatamu za uongozi
vi) Usimulizi wa nafsi ya kwanza-sisi tunataka
vii) Toni ya kushawishi na kushauri-kiongozi atakayeweza…
viii) Uradidi/takriri-kiongozi

Dondoo limetolewa uk. 40
Zozote 6x2=12

3b

i. Wanadumisha **amani** miongoni mwa wanafunzi. Mwalimu wa Ridhaa anazungumza na wanafunzi kuhusu umuhimu wa amani shuleni. Wanafunzi walikuwa wamemchokoza Ridhaa.
ii. Wanawafunza wanafunzi **maadili**. Mwangeka anakumbuka maneno ya mwalimu wake wa dini kuwa wawaheshimu wazazi wao.
iii. Wanatafuta **habari** zaidi kuhusu hali ya wanafunzi wao. Bi. Dhahabu alipata habari kuhusu Umu kutoka kwa mwalimu msimamizi wa darasa lake.
iv. Wanawatafutia wanafunzi wao **wazazi** wa kupanga. Kwa mfano Mwalimu dhahabu anampa Umu wazaza-Apondi na Mwangeka.
v. Wanawatafutia wanafunzi **mahali** pa kuishi/ makao. Bi. Tamasha anamtafutia Chandachema mahali pa kuishi-kwa Tenge na Kimai.
vi. Watu **wema**/wenye maelewano-mwalimu mkuu wa Kairu anamruhusu mama kulipa karo kidogo kidogo.
vii. **Wanawakomaza** wanafunzi wao wadogo akili kwa kuwafunza vizuri mambo ya kiuchumi na kisiasa kwa mfano Mwalimu Meli kwa kina Tila
viii. Wanasawiriwa kama **wasomi-**Fumba anajiongeza masomo na kuenda kufunza katika chuo kikuu.
ix. Wanatoa **ushauri** na uelekezaji kwa mfano Bw. Mwenge.
x. Wanadhihirisha **upendo** kwa wanafunzi. Bi. Dhahabu anampenda Umu. Anamkumbusha arejee darasani.

xi. Wanadhihirika kama wenye **bidii**-Walimu wa mwangeka waliwafunza masomo ya ziada.

xii. Wanasisitiza umuhimu wa **elimu** katika kuboresha maisha ya wanafunzi. Mwalimu Dhahabu kwa wanafunzi wake.

Zozote 8x1=8

(kumkweza mtu ni kumtukuza/kumsifu/kumpa sifa chanya)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

4a)

i) Majoka anawadhulumu Wanasagamoyo kwa kuwakosesha amani. Anatumia askari kuwapiga wanapoandamana. Mwishowe mkuu wa askari anamsaliti. Anamuunga mkono Tunu.

ii) Anamtuma Chopi kumwaangamiza Tunu. Chopi anamwamuru Ngurumo na Vijana wengine kumuua Tunu. Wanamvunja mguu. Mwanawe Majoka, Ngao Junior anapatika akiwa amefariki kutokana na Sumu ya Nyoka.

iii) Majoka anamuua Jabali ili asalie mamlakani. Wanasagamoyo, chini ya uongozi wa Tunu, wanamng'oa mamlakani.

iv) Ashua anawadharau na kujaribu kuwafukuza akina Tunu nyumbani kwake. Yanamwendea mrama watu wanapomgeuka na kuimwaga pombe yake.

v) Majoka anaruhusu matumizi ya dawa za kulevya katika shule yake. Wanafunzi wanageuka makabeji. Hawafuzu. Mwanawe, Ngao Junior, anafariki kutokana na dawa za kulevya.

vi) Chopi anamnyanyasa Sud pamoja na Mkewe Ashua. Kifo chake kinapangwa na Majoka na Sudi.

vii) Majoka anawanyanyasa Wanasagamoyo kwa kulifunga soko la Chapakazi na kuwafurusha. Soko linafunguliwa baadaye na Tunu. Majoka anaondolewa uongozini.husda anamvamia Ashua ofisini mwa Majoka kwa madai ya kumwendea kinyume na mmewe. Baadaye Majoka anakiri kuwa hampendi Husda.

viii) Husda anamvamia Ashua ofisini. Wote wanatiwa mbaroni licha ya kwamba Husda aliachiliwa huru baada ya muda mfupi.

Hoja 5x2; kadiria nyingine. Aonyeshe namna mtu alivyomtesa mwenzake naye pia akaishia kuteseka.

4b)

i) **Askari** wanatumiwa kuwatawanya wanapogoma na kuandamana. Wanapigwa na kuumizwa. Wengine wanauawa. Kwa mfano vijana watano.

ii) Majoka anatumia **vitisho** katika utawala wake. Anawatisha wanaompinga kama Tunu na Sudi.

iii) Majoka **anawaua** wapinzani wake kwa mfano Jabali.

iv) Anaw**akandamiza** kiuchumi ili wazidi kumtegemea kwa mfano kufungwa kwa soko kunamfanya Ashua kwenda kumwomba chakula.

v) Anawatumia **vikaragosi** kutekeleza amri zake. Vikaragosi hawa wanamshauri vibaya. Chopi anamshauri kutumia nguvu zaidi.

vi) Kukandamizwa **kielimu**. Anatoa elimu duni. Wanafunzi katika shule zake wanatumia dawa za kulevya. Hawazinduki ili kuipigania jamii.

vii) Watu wanatupiwa vijikaratasi **wahame** kwa kutomuunga mkono Majoka. Kwa mfano akina Siti.

viii) **Anawahonga** watu ili wamuunge mkono. Watu wake wanapitia mangweni na kuwanunulia vijana pombe.

ix) Anatoa kandarasi kwa njia ya **ubaguzi** ili wahusika waendelee kumpigania. Ngurumo anapewa kandarasi ili azidi kumhudumia majoka.

x) Wizi wa **kura**-Majoka haamini katika demokrasia. Anatishia kuiba kura.

xi) Kukandamizwa kwa **vyombo** vya habari. Anasema kuwa atafunga vyombo vyote kisalie kimoja.

xii) Kuwafukuza **wafadhili** wa Tunu. Anaahidi kuwafukuza wafadhili wa Tunu ili Tunu ashindwe kuikomboa jamii yake.

xiii) **Propaganda-**watu wa Majoka wanawachochea Tunu na Sudi. Wanadai kuwa wana mahusiano ya kimapenzi. Mke wa Sudi anaamini katika hii propaganda.

xiv) **Ushawishi** mkubwa wa kiuchumi-Majoka anajiweza. Ana hela na raslimali za kutatiza ukombozo. Anataka kumpa Ashua kazi katika moja kati ya shule zake.

10x1=10

5a)

i. Maneno ya **Ngurumo**.

ii. Kauli mbili: Ya kwanza anamwambia **Sudi**; Sudi alimwambia atafakari kauli kuwa Tunu alikuwa amekuja **kuogelea**, sio kuvua.

iii. Kauli ya pili Ngurumo anawaambia **sudi na Tunu** kuwa **ulevi** ni safari ya hatua kwa hatua.

iv.

v. Walikuwa **Mangwen**i/Kwa Asiya/Kwa Mamapima/Kwa Boza.

vi. Tunu na Sudi **walikataa** kunywa pombe Mangweni.

Dondoo ni la ukurasa wa 57

Zozote 5x1=5

5b)

i. Toni ya dharau/kubeza-sina muda wa kupoteza/mambo yasiyoniruzuku
ii. Toni ya kushauri-safari hii ni hatua kwa hatua.

1x2=2

5c)

i. Yanaendeleza maudhui ya **ulevi-**watu walikuwa kwenye makundi wakinywa pombe.
ii. Yanadhihirisha **madhara** ya pombe haramu-mtu II anaanguka.
iii. Ni katika mandhari haya ambamo Ngurumo anathibitisha kuwa ndiye **aliyemvunja** Tunu mkuu.
iv. Yanadhihirisha **ujasiri** wa Tunu. Alikutana na Ngurumo aliyemuumiza.
v. Uhusiano na **historia** ya wahusika inajitokeza katika mandhari haya. Tunu na Ngurumo walisoma humu.
vi. Yanaendeleza **ploti** ya tamthilia. Tunu anaimbiwa wimbo.
vii. **Uvunjaji** wa sheria unajitokeza. Asiya alipewa kibali cha kuuza pombe na Majoka.
viii. Yanadhihirisha **msimamo dhabiti** wa Tunu na Sudi-hawanywi pombe.
ix. Yanaonyesha **mabadiliko** katika maisha ya wahisika. Sitia aliacha ulevi.
x. Yanaonyesha **mustakabali** wa mgogoro kati ya Ngurumo na Majoka-hauishi.
xi. Yanaonyesha **ufisadi** wa Majoka na watu wake-wao huwanunulia vijana pombe haramu.
xii. Yanaibua **taharuki**. Tunu anawaalika katika mkutano. Si wazi ikiwa watu watahudhuria.

Zozote 4x2=8

3d)

Msemaji ni Ngurumo.

i. Ni mpenda starehe na anasa-anakunywa pombe kwa mama pima.
ii. Ni katili-ndiye aliyemvunja Tunu mguu.
iii. Mwenye mapuuza-anasema hana muda wa kupoteza.

iv. Mwenye kejeli-anamwambia Asiya kuwa siku hizi hatambui jina lake halisi…uk. 56
v. Mwenye dharau-anaidharau familia ya Tunu. Anasema hawana wasifu wowote.
vi. Mjinga-anasema kuwa Sagamoyo ni pazuri tangu soko lilipofungwa ilhali watu wanaumia.
vii. Mkali/mwenye hasira-anawaamuru akina Sudi waondoke-uk 62
viii. Mpyaro-anamwambia Sudi kuwa ametia ndani ya kirinda na Tunu.
ix. Mwenye kumbukumbu nzuri-anaukumbuka wimbo wa Dauki Kabaka na kuuimba.

Zozote 5x1=5

## SEHEMU D: USHAIRI

## 6

a)

i. Mama alimshauri nafsi neni kuwa wanaume ni wanyama.
ii. Asiingilie anasa kwa kuwa amevunja ungo.
iii. Akijitia maringo atatungwa mimba.
iv. Hata wanaume waje na pesa, asiwakubali.
v. Wakipiga magoti asiwakubali pia.
vi. Asifanye ngono; ni tendo la suna.
vii. Athamini elimu kwanza.
viii. Asizurure mitaani.
ix. Aende shuleni moja kwa moja akitoka shuleni.
x. Asiende vichochoroni kuwaona wanaume.
xi. Awe msikivu, assize anayoambiwa.
xii. Atafunzwa mambo mengine kuhusu mapenzi atafunzwa.
xiii. Aliwakataa kina Hamadi.
xiv. Karisa alimpa ujauzito.
xv. Nafsi neni alifukuzwa shuleni.
xvi. Karisa bado anasoma.
xvii. Nafsi neni ni mjamzito; anajikuna upele.

Zozote 5x1

b)

i. Vina-ukara; vina vya kati havina urari; vya mwisho vina urari.
ii. Vipande; mathnawi; kila mshororo una vipande viwili.
iii. Tarbia; kila ubeti una mishororo mine.

3x1=3

c) i) Inkisari – ngawa – ingawa

taonywa – utaonywa

umuhimu:kusawazisha mizani

ii) Tabdila – ukimbile – ukimbie

usikile – usikie

umuhimu: kuleta urari wa vina

iii) Kuboronga/kufinyanga/kubananga

- Ngono – ni tendo la suna, Amina sikimbilie
  Amina sikimbile ngono si tabia tendo la suna
- Kuzurura mitaani, si tabia njema ile
  Ile tabia ya kuzurura mitaani si njema

Umuhimu: Kuleta mahadhi/kulipa shairi mapigo ya kimziki

2x1=2

d) Mama yake mshauriwa alama 1

"Kama mamayo mzazi, nakuonya ukimbilie alama 1

e) Uwe mwana anayesikia/msikivu wa kuzingatia yafuatayo /mambo kuhusu mapenzi utaonywa shuleni /lakini nikiwa mama yako mzazi ninakuonya kimbele ujihadhari na wanaume kwa sababu ni wanyama 4x1=4

**MWONGOZO 102/3 2022 NNE.**

f)

i. Urudiaji wa vina-vina vya mwisho vimerudiwa(-le, ma)
ii. Urudiaji wa mishororo-lina kibwagizo; si watu waole vile, wanaume ni wanyama.
iii. Urudiaji wa maneno-neno mbele; 2:3, 3:2

g)

i. Usifanye anasa/mapenzi
ii. Wanaume ni hatari/wanaweza kuharibu maisha yako
iii. Tufanye mapenzi

# 7

(a)

i. lina beti
ii. kila ubeti lina mishororo ingawaje idadi inatofautiana katika kila ubeti
iii. lina mizani katika mishororo
iv. lina maneno machache
v. lina kipande
vi. baadhi ya mishororo ina muwala

4x1=4

(b) Fafanua toni ya utungo huu (alama 2)
Toni ya kusihi- “nikumbuke mwanangu”
Wosia/nasaha

1x2=2

(c) Huku ukitoa mifano, linganua kati ya mistari toshelezi na mistari mishata

Mistari toshelezi-mstari uliokamilika kimaana ilhali mstari mishata ni mstari usiokamilika kimaana
Mfano wa mstari toshelezi-Nikumbuke mwangu,
Mstari mishata-staftahi ya saa nane alasiri

Kutofautisha=2
Kuaja mifano=2

(d) Eleza maudhui yoyote matatu yanayojitokeza

i. Umaskini- Mrejelewa na mamake walipitia maisha magumu hapo awali" kumbuka nyakati zile mimi ni mamako tulivyojidamka.
ii. Ukengeushi-anafurahia vitu vya kigeni-magari,saa
iii. Ajira-Anarauka asubuhi kwenda kazini
iv. Bidii-Anatia bidii kazini na kuweza kumiliki mali-volvo

4x1=4

(e)

i. Lina beti sita
ii. Kila ubeti una mishororo tofauti
iii. Vina vyote si sawa.
iv. Lina mishata na mistari kifu.
v. Mizani ni tofauti katika kila mishororo

Zozote 4x1

## SEHEMU E: HADITHI FUPI

### 8a) Umuhimu wa Mazungumzo kati ya Sasa na Mbura katika Kujenga Hadithi ya Shibe Inatumaliza

i. Yanaibua suala la **ubadhirifu** wa mali ya umma-jungu linateremshwa kwa gari la ikulu uk.39
ii. **Ubinafsi** na ulafi unajitokeza-wana vyao kisha pia ni wenye vyetu uk. 40
iii. Yanaonyesha namna viongozi wanavyoshiriki katika ubadhirifu wa mali ya umma. Sasa anamwambia mbura wawahi chakula/walijaza vyakula kwenye sahani zao.
iv. Yanaidhihirisha **ufaafu** wa anwani-Wanakula lakini hawashibi. Uk. 41
v. Yanachimuza **madhara** ya kula sana-sukari, presha, saratani na kadhalika.
vi. Yanaonyesha umuhimu wa **vyombo** vya habari katika kukomesha hali ubadhirifu wa mali ya umma.-sasa alishtuka
vii. Yanaendeleza **ploti** ya hadithi-yanaibua masuala yanayoshughulikiwa katika hadithi. Swala la shibe kwa jumla.

Zozote 5x2=10

**8b. Namna Suala la Malezi Lilivyoshughulikiwa katika hadithi ya Tulipokutana Tena na Mtihani wa Maisha.**

**Tulipokutana Tena**

i. Wazazi wa Bogoa **wanayakwepa** majukumu ya ulezi na kumpokeza Bogoa Bi. Sinai.
ii. Wazazi wa Bogoa wanashindwa kumudu **mahitaji** ya kumsingi kutokana na umaskini wao kv sabuni.
iii. Walezi wa watoto **wanawadhulumu**. Bi. Sinai anamtumikisha Bogoa; anamchoma.
iv. Walezi **wanawabagua** watoto; watoto wengine wanasoma ilhali Bogoa hapelekwi shuleni. Anachoma mandazi.
v. Walezi **wanawatisha** watoto. Bi. Sinai anamwonya Bogoa dhidi ya kusema madhila aliyopitia mikononi mwake.
vi. Wazazi **wanawadanganya** watoto-Babake Bogoa anamdanganya kuwa angempeleka kwa marafiki zake ambao ni watu wazuri. Kumbe ni katili.-Bi. Sinai.
vii. Watoto **wanatengwa** na familia zao bila hiari yao-Bogoa analia san asana wanapotaka kumpeleka kwa marafiki zao lakini hasikizwi na wazazi. Uk. 114
viii. Baadhi ya wazazi **wanawasomesha** wanao. Kuna wanafunzi katika shule ambamo Bogoa aliuza mandazi.

5x1=5

**Mtihani wa Maisha**

i. Watoto wanapelekwa shuleni bila **kubaguliwa**. Babake Samueli anawasomesha ndugu zake wa kike. Pia Samweli anasomeshwa.
ii. Wazazi **kuamini** kuwa kufeli katika mtihani wa shuleni ni kufeli katika mtihani wa maisha. Kwa mfano babake Samueli anaamini alifeli mtihani. Anafaa kufa.
iii. Wazazi kuamini kuwa kusomesha mtoto wa **kiume** ndiko kunakoweza kuwakwamua kutoka katika lindi la umaskini. Babake Samueli anaamini kuwa kumsomesha Samweli kungemwopoa kutoka katik umaskini.
iv. Watoto **kuwadanganya** wazazi. Baba Samwuli haamini.
v. Mama Samueli anamwonyesha mwanawe **upendo**. Hataki ajiue.

vi. Watoto wanafahamu **hulka** za wazazi wao. Samueli anajua mama angemwelewa ilhali baba angempiga kinyama kwa kufeli mtihani.

vii. Watoto wanashiriki katika mahusiano ya kiholela wakiwa shuleni. Samueli na Nina.

viii. Wazazi wanajaribu kila juhudi kuwasomesha watoto wao hata katika hali ya **umaskini**. Baba Samueli anauza takribani kila kitu kuwasomesha.

**<u>MUKHTASARI WA UTAHINI WA VITABU 2018-2021</u>**

**<u>HADITHI FUPI</u>**

| **MWAKA** | **HADITHI** | **VIPENGELE** |
|---|---|---|
| 2021 | ***Masharti ya Kisasa( swali la 4)*** | i. Muktadha(uk. 56)-4<br>ii. Toni ya dondoo-2<br>iii. Misumari ya nyuki kwa kurejelea hadithi-14 |
| 2021 | ***Mame Bakari(swali la 5)*** | Suala la uozo wa kijamii-10 |
| 2021 | ***Ndoto ya Mashaka(swali la 5)*** | Mchango wa wazazi katika maisha ya vijana-10 |
| 2020 | ***Mwalimu Mstaafu (Swali la Lazima)*** | i) Muktadha(uk. 121)-4 |
| | | ii) Toni ya dondoo-2 |
| | | iii) Namna Jairo Alivyokitia Kitumbua Mchanga-10 |
| | | iv) Vipengele vya Kimtindo-4 |
| 2019 | ***Nizikeni Papa Hapa*** | Muktadha-4 |
| | | Mbinu za kimtindo-2 |
| | | Namna hadithi hii inavyohimiza uwajibikaji-6 |
| | ***Mapenzi ya Kifaurongo*** | Umaskini-8 |
| | ***Shogake Dada ana Ndevu*** | Unafiki-12 |
| | | Kuchanganua Mtindo-12 |
| 2018 | ***Mkubwa*** | Utabaka-12 |
| | ***Kidege*** | Utabaka-8 |
| <u>2018</u> | ***<u>Tumbo Lisiloshiba(swali la sita)</u>*** | i) <u>Dondoo(uk.2)</u> |
| | | ii) <u>Tamathali za Usemi-alama 3</u> |
| | | iii) <u>Sifa za Mzee Mago-alama 5</u> |

| | | |
|---|---|---|
| | | iv) <u>Namna Wanamadongoporomoka walivyolipukiwa na moto-alama 8</u> |

## <u>TAMTHILIA YA KIGOGO</u>

| <u>**MWAKA**</u> | <u>**VIPENGELE**</u> |
|---|---|
| 2021 | <u>**Swali la lazima**</u> |
| | a. i) Muktadha-alama 4, uk. 7 |
| | ii)vipengele vya kimtindo-2 |
| | iii) sifa za Kombe-4 |
| | b. kuzorota kwa maadili kunachangia kuzorota kwa mahusiano ya kijamii. |
| 2020 | **SWALI LA NNE** |
| | i) Muktadha wa dondoo-4(uk. 92) |
| | ii) Vipengele vya Kimtindo-4 |
| | iii) Umuhimu wa Asiya katika kujenga ploti na maudhui-12 |
| | **SWALI LA TANO** |
| | i) Mchango wa wasomi katika kuimarisha maisha ya Wanasagamoyo-10 |
| | ii) Umuhimu wa Mazungumzo kati ya Majoka na Daktari-10 |
| 2019 | **SWALI LA PILI** |
| | i) Mbinu walizotumia Wanasagamoyo Kupigana na utawala dhalimu-10 |
| | ii) Namna mbinu rejeshi ilivyotumiwa kujenga wahusika na maudhui-10 |
| | **SWALI LA TATU** |
| | i) Dondoo-4(uk. 26) |
| | ii) Dhima ya vipengele viwili vya Kimtindo-alama 4 |
| | iii) Sifa za Ashua-6 |

| | |
|---|---|
| | iv) Umuhimu wa Mandhari katika tamthilia hii-6 |
| 2018 | **SWALI LA NNE** |
| | i) Dondoo-4(uk. 5) |
| | ii) Kinyume katika dondoo-16 |
| | **SWALI LA TANO** |
| | iii) Dondoo(uk. 25)-umuhimu wa Ashua katika kujenga tamthilia-6 |
| | iv) Namna uongozi wa Majoka unavyoyazika matumaini ya Wanasagamoyo-14 |

**<u>RIWAYA YA CHOZI LA HERI</u>**

| **MWAKA** | **VIPENGELE** |
|---|---|
| **2021** | **Swali la Pili**: nafasi ya mwanamke katika kuendeleza ukiukaji wa haki za kibinadamu-alama 20 |
| | **Swali la tatu:** kuchanganua mtindo katika dondoo(uk. 91) na umuhimu wa Cizarina na Tila(alama 10) |
| **2020** | **SWALI LA PILI** |
| | Dondoo-4(uk. 153) |
| | Aina za **taswira**-4 |
| | Vipengele vya kimtindo-4 |
| | **Umuhimu wa mandhari** katika kujenga riwaya kwa kurejelea kituo cha mwanzo mpya. |
| | **SWALI LA TATU** |
| | Kuchanganua mtindo-dondoo(uk. 181)-8 |
| | **Mchango wa familia** katika katika kuendeleza desturi za jamii(rejelea kisa cha **Mwangeka, Mwangemi** na Babu yao) |

| | |
|---|---|
| **2019** | **SWALI LA LAZIMA** |
| | Dondoo-4(uk. 140) |
| | Tamathali mbilI za usemi-2 |
| | Umuhimu wa **Selume-**6 |
| | Mikakati wanayotumia vijana kupambana na hali zao(rej. **Chandachema na Dick)-**8 |

**MWALIMU ONYANGO. 0707311302.**

MWISHO.